**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TAARIFA KWA UMMA**

# KUHUSU UCHAGUZI WA MADIWANI KATIKA KATA YA MINDU JIMBO LA MOROGORO MJINI, KATA YA MZINGA JIMBO LA KIVULE NA KATA YA KIRUA VUNJO MAGHARIBI JIMBO LA VUNJO

**Dodoma, 24 Oktoba, 2025**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea taarifa kuhusu vifo vya wagombea wa udiwani watatu wa Kata ya Mindu, Jimbo la Morogoro Mjini, Kata ya Mzinga, Jimbo la Kivule na Kata ya Kirua Vunjo Magharibi, Jimbo la Vunjo kama ifuatavyo: -

1. Kifo cha Ndugu Hamisi Mohamedi Msasa, aliyekuwa mgombea wa Udiwani katika Kata ya Mindu, Jimbo la Morogoro Mjini kupitia Chama cha Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo) kilichotokea tarehe 17 Oktoba, 2025. Kwahiyo, Uchaguzi katika Kata hiyo ulisitishwa rasmi tarehe 17 Oktoba, 2025.

2. Kifo cha Ndugu Rashid Abdallah Nandonde aliyekuwa mgombea wa Udiwani katika Kata ya Mzinga, Jimbo la Kivule kupitia Chama cha The Civic United Front (CUF-Chama cha Wananchi) kilichotokea tarehe 19 Oktoba, 2025. Kwahiyo, Uchaguzi katika Kata hiyo ulisitishwa rasmi tarehe 19 Oktoba, 2025.

3. Kifo cha Ndugu John Boniface Kessy aliyekuwa mgombea wa Udiwani katika Kata ya Kirua Vunjo Magharibi, Jimbo la Vunjo kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilichotokea tarehe 21 Oktoba, 2025. Kwahiyo, Uchaguzi katika Kata hiyo ulisitishwa rasmi tarehe 21 Oktoba, 2025.

Hivyo, kutokana na vifo vya waliokuwa wagombea udiwani katika maeneo tajwa na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 68(1), (3) na (4) na 71(2) vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, Tume inatoa taarifa

UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura

kwa umma kuhusu ratiba ya uchaguzi wa Udiwani katika Kata ya Mindu, Kata ya Mzinga na Kata ya Kirua Vunjo Magharibi kama ifuatavyo: -

1. Fomu za uteuzi katika Kata ya Mindu, Kata ya Mzinga na Kata ya Kirua Vunjo Magharibi zitatolewa **tarehe 28 Oktoba, 2025 hadi 03 Novemba, 2025;**

2. Uteuzi wa wagombea Udiwani katika Kata ya Mindu, Kata ya Mzinga na Kata ya Kirua Vunjo Magharibi utafanyika **tarehe 03 Novemba, 2025;**

3. Kampeni za uchaguzi wa Madiwani katika Kata ya Mindu, Kata ya Mzinga na Kata ya Kirua Vunjo Magharibi zitafanyika kuanzia **tarehe 4 Novemba, 2025 hadi tarehe 4 Januari, 2026;**

4. Uchaguzi wa Madiwani katika Kata ya Mindu, Kata ya Mzinga na Kata ya Kirua Vunjo Magharibi utafanyika **siku ya Jumatatu tarehe 05 Januari, 2026.**

Uteuzi mpya hautahusisha mgombea mwingine yeyote aliyeteuliwa kihalali katika uteuzi uliofanyika awali isipokuwa kama atatoa taarifa ya kujitoa.

Tume inatumia nafasi hii kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na Maelekezo yatakayotolewa na Tume katika kufanikisha ratiba ya uchaguzi husika.

Imetolewa na:

Kailima, R. K
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

## "KURA YAKO HAKI YAKO JITOKEZE KUPIGA KURA"

**UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025**
Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura